LIC LOCAL INVESTMENT CLIMATE

**Brief No. 4**

# MAJADILIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI JUU YA MAENDELEO YA BIASHARA

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Kulingana na utafiti wa awali juu ya changamoto za biashara katika mikoa miwili (Kigoma na Dodoma) uliofanyika mwaka 2014, ulitambua kuwa hakuna jukwaa rasmi na sahihi la majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi au mifumo iliyopo katika ngazi za wilaya na mkoa pia haikuwa rasmi, mbali tu na amri ya rais ya kuanzisha mabaraza ya biashara ya wilaya. Kulingana na hili, mradi wa LIC umeanzisha msaada kwa ajili ya kuanzishwa kwa mabaraza ya biashara katika wilaya 16 za Dodoma na Kigoma na baraza la biashara la mkoa (RBC) katika mikoa yote miwili.

Malengo makuu ya kuanzisha jukwaa la majadiliano kama vile mabaraza ya biashara ya wilaya na baraza la biashara la mkoa ni kujenga imani kati ya wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi, kuandaa na kutekeleza sera na mipango ya kusaidia maendeleo ya biashara. Kwa njia ya majadiliano tu, sekta zote husika zinatambua na kuelewa manufaa ya ushirikiano wa pamoja wa kuaminika, wakiongozwa na maono yaliyokubaliwa kwa pamoja na ajenda ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Majadiliano pia yanatumika kutambua uwezekano wa fursa mpya za biashara ndani ya wilaya na mikoani kwa kushirikiana na kuendeleza mifano bora katika utoaji wa huduma (kwa sekta zote za umma na binafsi) ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato ya biashara yanayosimamiwa na mamlaka za serikali za mitaa.

**Miundo ya mabaraza ya biashara ya wilaya (DBCs) and mkoa (RBCs)**

Kulingana na miongozo ya namna ya kuendesha mabaraza ya biashara iliyotolewa na Baraza la Biashara la Taifa la Tanzania (TNBC), ushiriki kwenye mabaraza ya biashara ya wilaya (DBCs) unajumuisha wajumbe 20 kutoka kwenye kila sekta (sekta ya umma na sekta binafsi). Kamati tendaji ina wajibu wa kuandaa ajenda na muongozo wa jinsi ya kuendesha mabaraza ya biashara. Kamati tendaji pia ina uwiano sawa wa wawakilishi kutoka sekta zote mbili. Mabaraza ya biashara yanasimamiwa na mkuu wa wilaya kama mwenyekiti na kamati tendaji inayoongozwa na mkurugenzi wa halmashauri pamoja na muwakilishi kutoka sekta binafsi.
Wawakilishi kutoka sekta ya umma huchaguliwa kati ya wakuu wa idara zinazohusiana moja kwa moja na maendeleo ya biashara na kutoka kwenye taasisi husika za serikali katika ngazi za wilaya na mkoa. Wawakilishi wa sekta binafsi wanachaguliwa kutoka kwa mashirika ya sekta ya binafsi yaliyotambuliwa kwa kushirikiana na wilaya na mkoa husika.



Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma katika mkutano wa baraza la biashar katika Ukumbi wa Aqua Lodge



Eneo Jipya la kukaushia dagaa ambayo ni moja ya matunda ya PPDs kwa msaada wa LIC kupitia mradi wa kuboresha mwalo wa kibirizi na soko la samaki la kigoma

**Mafanikio makubwa kutokana na mchakato wa PPD**

- Uanzishwaji wa jukwaa rasmi la majadiliano katika ngazi ya wilaya (DBCs) katika wilaya zote za mikoa ya Dodoma na Kigoma
- Uanzishwaji wa jukwaa rasmi la majadiliano katika ngazi ya mkoa (RBCs) katika mikoa Dodoma na Kigoma
- Mchango mkubwa wa uzoefu kuhusu masuala ya PPD kutoka kwenye mradi wa LIC, mapitio na uundaji wa miongozo mipya ya PPD kitaifa umefanyika na kuratibiwa na Baraza la Biashara la Taifa la Tanzania (TNBC)
- Ushiriki wa sekta binafsi kwenye maandalizi ya bajeti katika mamlaka za serikali za mitaa mfano; Kongwa na Mpwapwa
- Kutokana na matokeo mazuri ya uhusiano na uaminifu ambao umeanzishwa baina ya sekta umma and sekta binafsi katika ngazi ya wilaya, uwekezaji mpya na ubunifu katika uwekezaji umeibuliwa, kwa mafano: kituo maalumu cha biashara ya kuku wilayani Kongwa (Local Chicken Hub), vituo vya vyashara katika wilaya zote za Kigoma na Dodoma, uboreshaji wa mwalo na soko la samaki la Kibirizi mkoani Kigoma, uendelezaji wa Kituo cha kilimo cha Kibakwe wilayani Mpwapwa katika Mkoa wa Dodoma na kuundwa kwa sheria mpya ya kupunguza tozo za mazao.
- LIC inasaidia mashirika ya sekta binafsi katika mikoa yote miwili kuweza kujitayarisha vyema katika ushiriki wao kwenye majadiliano hasa kupitia ushirikishwaji wao kwenye mabaraza ya biashara. Kupitia msaada huu, sekta binafsi imejijenga zaidi na ushirikiano wao na sekta ya umma umesaidia kukuza hali ya ubora wa biashara katika mikoa yote miwili na kwa faida ya pande zote mbili.
- Muda unaotumika kusajili biashara umepungua kwa kiasi kikubwa sana wastani wa siku saba hadi siku mbili katika mikoa Kigoma na Dodoma
- Mchakato wa jukwaa la majadiliano (PPD) umesaidia kuboresha ubora wa ushauri unaotolewa na sekta binafsi kwa serikali za mitaa
- Msaada kwa sekta za umma katika ushiriki wa majadiliano ya pamoja unajumuisha kuimarisha mamlaka za serikali za mitaa uwezo wa kuongeza ukusanyaji wa mapato bila kuumiza maendeleo ya biashara.




Kituo cha Biashara – Chamwino, Dodoma




Kituo cha Biashara – Uvinza, Kigoma

**Kituo cha Biashara**

LIC imesaidia ujenzi pamoja na samani katika vituo vya biashara kwenye wilaya /manispaa /halmashauri za mji katika mikoa yote miwili. Vituo hivi vya biashara vitakuwa sehemu ambayo jamii ya wafanyabiashara watakuwa na uwezo wa kupata habari za masoko na biashara, huduma za kisheria, usajili wa ardhi, ushauri and muongozo wa masuala ya kodi na huduma za kibenki.

Mradi wa LIC umewekeza takriban Tshs bilioni 1.4 kwenye ujenzi / ukarabati wa vituo vya biashara ikiwa ni pamoja na usambazaji wa samani na vifaa vya komputa na mtandao. Uwekezaji huu ni pamoja na msaada endelevu wa kuwezesha jukwaa la majadiliano na miradi mengine ya maendeleo ya sekta binafsi katika mikoa hii miwili.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.ot.tz

**Oktoba 2018**